

Kugawa makundi

- Andaa mzinga mpya
- Kata nusu ya masega toka kiota cha zamani na kuweka kwenye mzinga mpya
- Chukua sehemu ya chakula (asali na chavua) kutoka kiota cha zamani na kuweka kwenye mzinga mpya. Funika mizinga yote.
- Weka mzinga mpya kwenye eneo ulipokuwa mzinga wa zamani.
- Weka mzinga wa zamani eneo jipya, lazimma iwe umbali wa zaidi ya mita hamsini toka ulipo mzinga wenye kiota kipya.

Kiota cha nyuki wasiouma



Uvunaji wa asali

- Funua mzinga kwa uangalifu, usiharibu kiota
- Vuna asali iliyokomaa kwa kutoboa vyungu
- Inamisha mzinga na mimina asali vizuri
- Nyunyizia unga wa ulezi ili kukausha unyevu
- Zingatia usafi na usipakaze asali nje ya mzinga
- Funika mzinga na urudishie mahali pake pa mwanzo
- Bakiza asali ya akiba ya nyuki

Kwa mawasiliano zaidi;
Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania
Kituo cha Utafiti wa Wanyamapori Njiro
Box: 661 Arusha, Tanzania
Simu: +255 27 254 9571
Barua pepe: nwrc@tawiri.or.tz



UFUGAJI WA NYUKI WASIOUMA



“Nyuki wasiouma wanafugika na hutoa asali yenye soko kubwa”

Aina ya mizinga

1. Mizinga ya magogo



- Wafugaji wengi wa jadi hutumia mizinga ya magogo kwa ufugaji huu
- Mizinga hii huvunwa kwa ugumu kuliko mizinga iliyoboreshwa
- Ni vigumu kuhuisha ujazo kwa aina hii ya mizinga

2. Mizinga iliyoboreshwa



- Mizinga ya masanduku ni rahisi zaidi kwa matumizi, hasa wakati wa kuhamisia ama kugawa makundi, na pia kwenye uvunaji

Jinsi ya kupata makundi



1. Kuhamisha kundi toka kiota cha asili kwenda kwenye mzinga

- Tafuta nyuki kwenye viota vya asili
- Kata gogo la mti futi moja pande zote 2 tokea kwenye tundu la mlango
- Hamishia gogo kwenye eneo unalotaka kuwahamishia nyuki
- Acha gogo kwa siku kadhaa
- Hamisha nyuki (mchana au wakati wa joto) toka kwenye kiota cha asili kwenda kwenye mzinga ulioandaliwa

lisha makundi

- Weka mzinga kwenye eneo lilipokuwa limewekwa gogo
- Lisha kundi kwa kumia asali yao wenyewe
- Unaweza kutumia unga wa ulezi au mahindi. Unga huu hutumika kama chakula, na pia husaidia kukausha asali iliyomwagika kwenye mzinga wakati wa kugawa ama kuhamishia kundi..

Ikumbukwe kuwa nyuki wakizama kwenye asali iliyomwagika kwenye mzinga hushindwa kuruka, na pia asali hiyo yaweza kuvutia maadui kama sisimizi

Kulisha kundi

